**MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO KILICHOFANYIKA TAREHE 12/11/2021 KATIKA UKUMBI WA MKUTANO WA KITUO CHA BIASHARA HALMASHAURI YA WILAYA YA UVINZA.**

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA:**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Jackson F.Mateso - | Diwani kata ya Kalya | -Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Salvatory M.Mkozi - | Diwani kata ya Mtegowanoti | -M/M/kiti |
| 3. | Mhe. Sibonja R.Masoud - | Diwani kata ya Buhingu | -Mjumbe |
| 4. | Mhe. Seleman R. Mswago - | Diwani kata ya Igalula | -Mjumbe |
| 5. | Mhe.Dickson D.Gube - | Diwani kata ya Nguruka | -Mjumbe |
| 6. | Mhe. Nuru I.Kashakali - | Diwani kata ya Kazuramimba | -Mjumbe |
| 7. | Mhe.Asia A.Dodo - | Diwani V/Maalum Ilagala | -Mjumbe |
| 8. | Mhe. Felista T.Kiteme - | Diwani V/Maalum Sunuka | -Mjumbe |
| 9. | Mhe. Tatu H.Rashidi - | Diwani V/Maalum Kalya | -Mjumbe |
| 10. | Ndg.Kechegwa.H.Masumbuko- | K/Mkurugenzi Mtendaji (W) | -Katibu |

**WATAALAM WALIOHUDHUIA:**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Ndg, Upendo Marango - | Katibu Tawala (W) |
| 2. | Ndg, Zabibu Mkamba - | Afisa Utumishi (W) |
| 3. | Ndg, Gervas Lupembe - | Afisa Mipango (W) |
| 4. | Ndg, Hilary Bitwaye - | Afisa Elimu ya Msingi(W) |
| 5. | Ndg, Nyakiha John - | Mkaguzi wa Ndani (W) |
| 6. | Ndg, Isack Masenya - | Kaimu Afisa Elimu ya Sekondari(W) |
| 7. | Ndg,Nteminyanda Kabengwe- | Kaimu Mweka Hazina(W) |
| 8. | Ndg, Samwel Wagala - | Kaimu Afisa Mifugo na Uvuvi (W) |
| 9. | Ndg,Kingu M. Danford - | Kaimu Afisa Maendeleo ya Jamii(W) |
| 10. | Ndg,Ibrahimu Mafuwe - | Kaimu Afisa TEHAM(W) |
| 11. | Ndg,Cyprian Nzamba - | Mratibu TASAF(W) |
| 12. | Ndg,Godfrey Baryorugulu - | Kaimu Afisa Biashara(W) |
| 13. | Ndg,Zacharia Mzese - | Kaimu Mwanasheria(W) |
| 14. | Ndg, Hussein Kateranya - | Kaimu Afisa Mazingira(W) |
| 15. | Ndg,Manyama Makongo - | Kaimu Afisa Ardhi(W) |
| 16. | Ndg,Bosco, George - | Kaimu Afisa Usafirishaji(W) |
| 17. | Ndg,Ester Gwiboha - | Kaimu Afisa Manunuzi(W) |
| 18. | Ndg, Philipo Marco - | Kaimu Mhandisi Ujenzi(W) |
| 19. | Ndg, Dr. Deogratiaus Mlandali- | Kaimu Mganga Mkuu ((W) |
| 20. | Ndg,Eustadius Rwezaula - | Afisa Tarafa ya Buhingu |
| 21. | Ndg, Liwaza Msasa - | Afisa Tarafa ya Ilagala |
| 22. | Ndg,Boniface Bahingayi - | Kaimu Afisa Tarafa ya Nguruka |
| 23. | Ndg, Justin R.Kapama - | Kaimu Afisa Nyuki (W) |



Scanned with CamScanner

**SEKRETARIETI**

1. Ndg. Evarist N.Bareguye - Mwandishi wa Vikao
2. Ndg. Charles Robert - Mwandishi wa Vikao

**AGENDA NA. 01: MUHT. NA. 20/2021/2022 KUFUNGUA KIKAO**

Kabla ya kumkaribisha Mwenyekiti afungue kikao, katibu alitoa taarifa kwamba, akidi ilikuwa imetimia na kikao kilikuwa cha kawaida. Aidha alitoa udhuru wa Mkurugenzi Mtendaji na Mweka Hazina kutoshiriki kikao baada ya kuwa na majukumu mengine ya kiutendaji. Katibu aliendelea kutoa taarifa kuhusu uhamisho wa Afisa elimu ya sekondari na Afisa elimu ya msingi na pia kupokelewa kwa Afisa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika, Afisa elimu ya msingi na Afisa elimu ya sekondari ambao wamehamia Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza. Baada ya maelezo hayo, katibu alimkaribisha Mwenyekiti, Mwenyekiti alifungua kikao rasmi saa 3.15 asubuhi kwa kuwakaribisha wajumbe wote wa kikao na kusisitiza kuwa, miradi yote ya maendeleo hususan ya idara ya elimu ya msingi kwamba, isimamiwe kwa ukaribu kuhakikisha inatekelezwa na kukamilishwa kwa wakati.

**AGENDA NA. 02: MUHT. NA. 21/2021/2022 KUTHIBITISHA AGENDA**

Agenda zilisomwa na kuthibitishwa na wajumbe wote bila kufanya mabadiliko yoyote.

1. Kufungua kikao.
2. Kuthibitisha agenda.
3. Kusoma na kuthibitisha Muhtasari wa kikao cha tarehe 11/10/2021.
4. Yatokanayo na Muhtasari wa Kikao cha tarehe 11/10/2021.
5. Taarifa ya Mapato na Matumizi ya mwezi Julai hadi Septemba, 2021.
6. Taarifa ya ukaguzi kipindi cha robo ya kwanza Julai hadi Septemba, 2021.
7. Taarifa ya utekelezaji wa miradi ya Maendeleo kipindi cha robo ya kwanza julai hadi septemba, 2021.
8. Taarifa ya idara ya utawala na utumishi pamoja na vitengo kwa kipindi cha robo ya kwanza julai hadi septemba,2021.
   - ✓ Idara ya utawala
   - ✓ Kitengo cha Manunuzi.
   - ✓ Kitengo cha TEHAMA.
   - ✓ Kitengo cha Sheria.
9. Kufunga kikao.

Scanned with CamScanner

**AGENDA NA. 03: MUHT. NA.22/2021/2022 KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 11, NOVEMBA, 2021.**

Wajumbe walipitia muhtasari wa kikao cha tarehe 11/10/2021 ukurasa kwa ukurasa kisha waliridhia muhtasari huo usainiwe na kuwa kumbukumbu sahihi ya kikao cha tarehe 11 Novemba, 2021.

**AGENDA NA. 04: MUHT. NA. 23/2021/2022 YATOKANAYO NA KIKAO CHA TAREHE 11/10/2021.**

Mwenyekiti alitoa nafasi kwa Katibu aweze kuwapitisha wajumbe kwenye yatokanayo na kikao cha tarehe 11/10/2021. Baada ya uwasilishwaji wa yatokanayo na kikao kilichopita, Wajumbe walipata fursa ya kujadili masuala mbalimbali yatokanayo na kikao hicho kama ifuatavyo:-

**AGENDA NA. 04: MUHT. NA.16/2021/2022**

**AZIMIO**

Mkaguzi wa ndani apitie vitabu vya michango ya ujenzi wa vyumba vya madarasa shule ya Sekondari Lagosa kujiridhisha matumizi ya fedha kisha awasilishe taarifa kikao kijacho.

**UTEKELEZAJI**

Taarifa ya ukaguzi wa mapato na matumizi ya michango ya kuchangia ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa shule ya sekondari Lagosa kata ya Igalula ilijadiliwa na iliazimiwa kama ifuatavyo:-

**AZIMIO.**

Kupitia taarifa ya mkaguzi wa ndani, hatua zichukuliwe, Afisa Utumishi ashughulikie taarifa itolewe kikao kijacho.

**AGENDA NA. 04: MUHT. NA.16/2021/2022**

**AZIMIO**

Mkurugenzi akutane na uongozi wa TPA ili kupata ufafanuzi wa suala la ukusanyaji wa fedha ya kikanyaga mchanga kiasi cha Tshs.5000/= ili fedha hizo zikusanywe na Halmashauri pamoja na suala la tozo zinazochangishwa bila kutolewa risiti.

**UTEKELEZAJI.**

Kikao cha Wakuu wa idara na TASAC kilikaa tarehe 20/10/2021 na kujadili suala hili ilifahamika kuwa, ushuru wa kikanyaga mchanga ni suala ambalo lipo chini ya mamlaka ya ofisi ya Uhamiaji ambalo liliwasilishwa kwa Mkuu wa Wilaya. Aidha Halmashauri baada ya kikao hicho ilipanga kuingia mkataba na TASAC kukusanya mapato kwenye maeneo ambayo Halmashauri haiwezi kufika na kukusanya kwa maana ya maeneo ambayo TASAC inamamlaka pekee ya kukusanya mapato kwa mujibu wa taratibu za kisheria.



Scanned with CamScanner

Suala hili liliendelea kujadili kwamba endapo kamati itaridhia TASAC watasaidia kukusanya mapato kwenye maeneo ya mamlaka yao yanayoruhusiwa kisheria hususan upotevu wa mapato ya Halmashauri kwenye maboti ya kwenda nje ya nchi.

**AGENDA NA. 04: MUHT. NA.16/2021/2022**

**AZIMIO**

Taarifa kuhusu eneo la "Rest House" ya Nguruka iwasilishwe kwa wajumbe ikifafanua eneo linaukubwa gani na kwa nini linapungua.

**UTEKELEZAJI.**

Mchoro unaoonesha eneo la "Rest House", kituo cha Polisi na shule ya msingi uliwasilishwa kwa wajumbe. Wajumbe waliendelea kujadili suala hili na iliazimiwa kama ifuatavyo:-

**AZIMIO.**

Taarifa kuhusu eneo la "Rest House" ya Nguruka iwasilishwe ikionesha eneo lina ukubwa gani.

**AGENDA NA. 04: MUHT. NA.16/2021/2022**

**AZIMIO**

Mwanashaeria afungue kesi kudai jengo la soko la Kazuramimba na afuatilie kufahamu kama wafanyabiashara wameondolewa na Afisa Mtendaji anakusanya ushuru wa Vizimba vya Soko.

**UTEKELEZAJI.**

Taarifa ilitolewa kwamba, nyaraka za kukata rufaa zimekwisha andaliwa. Suala hili lilijadiliwa ambapo wajumbe walitoa hoja kwamba, kama suala hili limeshindikana kushughulikiwa kiwilaya menejimenti ieleze, kwa kuwa mapato ya soko la Kazuramimba yanaendelea kupotea. Baada ya majadiliano iliazimiwa kama ifuatavyo:-

**AZIMIO**

Katika kikao kijacho taarifa iwasilishwe ikieleza ni maeneo gani katika soko la Kazuramimba yana mgogoro na ambayo hayana mgogoro pia ifahamike nyaraka za kukata rufaa zimefikia hatua gani.

**AGENDA NA. 04: MUHT. NA.16/2021/2022**

**AZIMIO**

Mkurugenzi Mtendaji atembelee maeneo yote ambayo yalitembelewa na waheshimiwa madiwani wakati wa ziara ya kukagua miradi na awasilishe mrejesho kwa wajumbe.



Scanned with CamScanner

**UTEKELEZAJI.**

Ziara ilikuwa bado inaendelea, taarifa itawasilishwa baada ya ziara kukamilika, wajumbe lipokea na kushauri litekelezwe na likamilishwe.

**AGENDA NA. 05: MUHT. NA. 24/2021/2022**

**AZIMIO**

Mweka Hazina awasilishe kwa wajumbe taarifa ya POS

1. Orodha ya wakusanya mapato wanaodai Halmashauri.
2. Orodha ya wakusanya mapato wanaodaiwa na Halmashauri.

**UTEKELEZI**

Orodha ya watoza ushuru iliwasilishwa kwa wajumbe ikionesha kiasi anachodaiwa na kiasi anachodai. Wajumbe walipokea na kujadili suala hili kwamba, ilikuondoa madeni ya watozo ushuru, Mtoza ushuru anapowasilisha fedha alipwe siku hiyo hiyo. Aidha baada ya wajumbe kupitia orodha hiyo iligulika kwamba, kiasi cha fedha ambacho watoza ushuru wanachodai Halmashauri ni kidogo kuliko wanachodaiwa na Halmashauri. Baada ya majadiliano iliazimiwa kama ifuatavyo:-

**AZIMIO**

- Watoza ushuru wanaoidai Halmashauri walipwe 50% kwa kupunguza.
- Watoza ushuru wanaodaiwa na Halmashauri wachukuliwe hatua kuhakikisha wanalipa fedha wanazodaiwa.

**AGENDA NA. 05: MUHT. NA.24/2021/2022 TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI MWEZI JULAI HADI SEPTEMBA, 2021.**

Taarifa ya mapato na matumizi ya mwezi Julai hadi Septemba, 2021 iliwasilishwa kwa wajumbe kuwa, Halmashauri kwa kipindi cha mwezi julai hadi septemba imekusanya jumla ya tshs 493,532,181.70 kutoka katika vyanzo mbalimbali vya mapato na ilikuwa na matumizi ya tshs 35,035,870,003.00 kwa mchanganuo ufuataao:-

Matumizi ya fedha za mapato ya ndani tshs 275,772,728.50

Matumizi ya ruzuku ya kawaida na mishahara tshs 4,588,167,352.74

Matumizi ya ruku ya maendeleo na fedha za wafadhili tshs 363,427,193.34

Wajumbe walipokea na walipitia taarifa ukurasa kwa ukurasa kisha walipitisha taarifa ya mwezi julai hadi septemba, 2021.



Scanned with CamScanner

**AGENDA NA. 06: MUHT. NA.25/2021/2022 TAARIFA YA UKAGUZI KIPINDI CHA ROBO YA KWANZA MWEZI JULAI HADI SEPTEMBA, 2021.**

Mwenyekiti alitoa nafasi kwa Katibu aweze kuwapitisha wajumbe kwenye taarifa ya ukaguzi kipindi cha robo ya kwanza mwezi Julai hadi Septemba, 2021 ambaye alimkaribisha mkaguzi awasilishe taarifa kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji. Baada ya uwasilishwaji wa taarifa ya ukaguzi, Wajumbe walipata fursa ya kujadili masuala mbalimbali katika taarifa hiyo kwa kupia ukurasa kwa ukurasa na kutoa maoni kama ifuatavyo:-

Hoja Na.1.1 Malipo yenye nyaraka pungufu.

**Maoni ya Kamati.**

Kamti iliunga mkono maoni ya kamati ya ukaguzi na kujadili kuhusu

Hoja ilihusu malipo ya kukwamua gari huko Mgambo tshs 550,000/= ambapo iliazimiwa kama ifuatavyo:-

**AZIMIO**

1. Hoja ya malipo ya kukwamua gari huko Mgambo kwa tshs 550,000/= iwasilishwe kikao kijacho bila kuongeza nyaraka nyingi ambazo hazikuwasilishwa ndani ya kikao hiki.

2. Majina ya wanaohusika na hoja hii yawasilishwe kwenye kikao kijacho.

Hoja Na.1.2. masurufu ambayo hayakuandikwa kwenye daftari la masurufu aidha hayajarejeshwa kiasi cha shilingi 46,197,400.00

**Maoni ya Kamati.**

Kamati iliunga mkono maoni ya kamati ya ukaguzi ya kwamba, daftari liandaliwe na masurufu yarejeshwe ndani ya mwezi mmoja kuanzia tarehe 9/11/2021.

Hoja Na. 2.0 shule za msingi.

2.1.Shule ya Msingi Kachilingulu.

2.1.1.Mali/bidhaa zilizotolewa stoo bila kutumia hati ya kutolea mali/bidhaa stoo.

**Maoni ya Kamati.**

Kamati ilunga mkono maoni ya kamati ya ukaguzi.

Hoja Na.3.0 Shule ya Msingi Nguruka

3.1 Malipo kwa madawati ambayo hayakupokelewa shuleni

**Maoni ya Kamati.**



Scanned with CamScanner

Kamati iliunga mkono maoni ya kamati ya ukaguzi

Hoja Na.4.0 Shule za sekondari

4.1. Shule ya sekondari Nguruka

4.1.1.Malipo nyenye shaka kiasi cha tshs 2,172,700.00

**Maoni ya Kamati.**

Kamati iliunga mkono maoni ya kamati ya ukaguzi.

4.2. Shule ya Sekondari Ruchugi

4.2.1. malipo kwa watahiniwa ambayo haikupelekwa shuleni

**Maoni ya Kamati**

Kamti iliunga mkono maoni ya kamati ya ukaguzi

5.0 Kituo cha Afya Nguruka

5.1.Sehemu ya malipo ya kiti cha kung'olea meno ambayo hayakufuata taratibu za manunuzi shilingi 9,102,042.59

**Maoni ya Kamati-** kamati ilijadilili na iliazimia kama ifuatavyo:-

**Azimio**

Ufafanuzi kuhusu manunuzi ya Kiti cha kung'olea meno Tshs 9,102,042.59 uwasilishwe kwa wajumbe kikao kijacho.

5.2 kiasi cha fedha ya mauzo ya dawa na malipo ya papo kwa papo ambacho hakikupelekwa benki kuanzia tarehe 18/08/2021 hadi 9/10/2021 kiasi cha tshs 1,979,250.00

**Maoni ya kamati**

Kamati iliunga mkono maoni ya kamati ya ukaguzi.

6.0. Kituo cha Afya Ilagala

Malipo yenye shaka kwa ukarabati wa kichomea taka(Incinerator) shilingi 1,592,426.52

**Maoni ya Kamati**

Kamati iliunga mkono maoni ya kamati ya ukaguzi.



Scanned with CamScanner

**AGENDA NA. 07: MUHT. NA.26/2021/2022 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 HADI KUFIKIA MWEZI SEPTEMBA.**

Mwenyekiti alitoa nafasi kwa Katibu aweze kuwapitisha wajumbe kwenye taarifa ya utekelezaji wa miradi ya mendeleo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 hadi kufikia mwezi septemba ambaye alimkaribisha Afisa Mipango na Takwimu awasilishe taarifa kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji ambapo taarifa ilieleza kwamba, Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2021/2022 imepanga kutekeleza miradi yenye dhamani ya tshs 16,079,256,080 ambapo kiasi cha Tsh 6,048,858,080 ni fedha za ndani na Tshs 10,030,398,000/= ni fedha za wafadhili. Hadi kufikia mwezi septemba Halmashauri haijapokea fedha toka Serikali Kuu kama ilivyopitishwa na Bunge.Halmashauri imepokea fedha nje ya bajeti tsh 250,000,000 tozo ya miamala ya simu kwa ajili ya ukamilishaji wa kituo cha Afya Ilagala,ukamilishaji wa vyumba vya madarasa shule ya sekondari Mazungwe na Sunuka Tshs 50,000,000/= ukarabati wa mnada wa mifugo toka UNCDF TSHS 161,536,920/= imepokea tshs 66,748,000/= toka TASAF. Aidha imepokea tshs174,818,315.14 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa, nyumba ya mwalimu,maabara,ujenzi wa matundu ya vyoo na mifumo ya maji tshs 27,428,121/= kwa ajili ya UVIKO – 19 . Pia imepokea tshs 3,920,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 118 vya madarasa shule za sekondari na vyumba 78 katika shule shikizi. Wajumbe walipokea taarifa na walijadili, wajumbe walishauri vifaa vitakapopelekwa maeneo ya ujenzi, mheshimiwa diwani apewe taarifa hususan wakati wa mapokezi. Pia walisistiza ushirikishwaji wa Serikali ya kijiji katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Baada ya majadiliano na ushauri huo taarifa ilipokelewa na iliazimiwa kama ifuatavyo:-

**AZIMIO**

- Kila Mheshimiwa Diwani apokee barua ya kumtambulisha kwenye mradi husika kwenye kata yake.



Scanned with CamScanner

**AGENDA NA. 08: MUHT. NA.27/2021/2022 TAARIFA YA IDARA YA UTAWALA POMOJA NA VITENGO KWA KIPINDI CHA ROBO YA KWANZA JULAI HADI SEPTEMBA, 2021.**

Mwenyekiti alitoa nafasi kwa Katibu aweze kuwapitisha wajumbe kwenye taarifa ya shughuli zilizotekelezwa na idara ya Utumishi na Utawala pamoja na vitengo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 hadi kufikia mwezi septemba ambaye alimkaribisha Afisa Utumishi na Utawala,awasilishe taarifa kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji. Baada ya uwasilishwaji Wajumbe walipata fursa ya kujadili masuala mbalimbali katika taarifa ukurasa kwa ukurasa kama ifuatavyo:-

**Uhamisho wa watumishi.**

Wajumbe walishauri kabla ya kumhamisha mtumishi hususan watendaji wa kata na vijiji ofisi ya utumishi ijiridhishe kama mtumishi huyo hana changamoto yoyote ya kiutendaji.Afisa Utumishi atemebelee watendaji wa Karago na Mgambazi kuona wanachangamoto gani kwenye maeneo yao ya kiutendaji. Baada ya wajumbe kujadili, iliazimiwa kama ifuatavyo:-

**AZIMIO.**

Afisa Utumishi atemebelee watendaji wa Karago na Mgambazi kuona wanachangamoto gani kwenye maeneo yao ya kiutendaji.

**TAARIFA ZA VITENGO**

Taarifa ya kitengo cha sheria, TEHAMA na manunuzi ziliwasilishwa na kupitishwa na wajumbe wote. Aidha wajumbe walishauri katika kipindi kijacho taarifa ya kitengo cha uchaguzi iwasilishwe kwa kuwa zipo chaguzi zimekwama.

**AGENDA NA. 09: MUHT. NA. 28/2021/2022 KUFUNGA KIKAO**

Kabla ya kumkaribisha Mwenyekiti afunge kikao, Katibu aliwashukuru wajumbe wote kwa michango yao kisha alimkaribisha Mwenyekiti ambaye aliwashukuru wajumbe na washiriki wote kwa kushiriki kikamilifu katika kikao hicho. Pia alimkaribisha makamu Mwenyekiti ambaye alieongelea suala la vitambulisho vya NIDA kwamba bado ni tatizo kwa wananchi.



Scanned with CamScanner

Mwenyekiti alimkaribisha pia Katibu Tawala Wilaya ambaye aliwashukuru wajumbe kwa namna walivyoshiriki kwenye kikao. Baada ya hayo Mwenyekiti alifunga kikao saa 7.02 mchana kwa kusisitiza kwamba yote yaliyojadiliwa na kutolewa maamuzi katika kikao hicho yatekelezwe kwa ufanizi zaidi.

**UMETHIBITISHWA**

| | |
|---|---|
| ........................ | ........................................ |
| **MWENYEKITI** | **KATIBU** |

**TAREHE**......23/12/2021......



Scanned with CamScanner